

15-Miym Saakinah

Miym saakinah: Ni herufi ya م (miym) isiyokuwa na *i'raab* na ambayo ina sukuwn iliyothibiti wakati wa kuendelea kusoma au kusimama.

Inaweza kutokea katika nomino au kitenzi au kihusishi au kishirikishi.

Inaweza kuwa katikati ya neno au mwisho wa neno.

Hukmu za Miym Saakinah (م)



Idhwhaar Ash-Shafawiy

Ikhfaa Ash-Shafawiy

Idghaam Ash-Shafawiy

Hukmu za miym saakinah zimenasibishwa na 'Ash-Shafawiy' kwa vile herufi ya miym inatoka katika makhraj ya Ash-Shafataan (midomo miwili); kwa hiyo mfano inaposemwa ni "idghaam ash-shafawiy", ina maana ni idghaam inayotokea katika midomo miwili.